

Jina Nambari yako :

102/2

KISWAHILI

KARATASI 2

LUGHA

JULAI/AGOSTI 2014

MUDA: SAA 2 $\frac{1}{2}$

MTIHANI WA MWIGO WA KAUNTI NDOGO YA NYAMIRA

Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari Kenya (K.C.S.E)

102/2

Kiswahili

Karatasi 2

2 $\frac{1}{2}$

MAAGIZO

- Andika **jina lako** na **namba yako** katika nafasi ulioachiwa hapo juu.
- Jibu maswali yote.
- Andika majibu yako katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
Jumla	80	

Karatasi hii ina kurasa 8 zilizopigwa chapa. Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

1. UFAHAMU

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata

Wahenga walisema majembe yakikaa pamoja hayaachi kugongana. Methali hii imekaririwa kuonyesha migongano na migogoro baina ya viumba vyenye uhai hasa adinasi. Hii ndio sababu kuna sheria au amri ambazo hutuzunguka. Aghalabu mtu azikiukapo, anatwaliwa na hisi na hii ya ndani sana inaoweza kupima kiakili ifaayo. Mtu anaposhindwa, hisi hiyo humtawala kwa sheria au kuwekewa mipaka ambayo unapoivuka unhesabika kuwa wafanya inadi, ambapo ni sharti uadhibiwe.

Mambo haya hata hivyo yamekuwa hadithi siku hizi. Sheria zetu za leo zillibuka wakati wa ukoloni lakini zimefanyiwa marekebisho kadhaa, baada ya muda Fulani. Jamii zetu za kijadi hazikuwa zinaishi hobelahobela. Zilitawaliwa na mwongozo Fulani. Miongozo ilitofautiana kutoka sehemu moja hadi nyingine. Miongozo hii ilitolewa kwa wanajamii tangu wakiwa wadogo sana na hatua hiyo iliendelezwa hadi walipokomaa. Badala ya kuweka misahafu ya amri na sheria zenye kuandamanishwa na adhabu ya vifungo gerezani, faini na nyingine nyingi, miongozo hiyo ya kijamii ilitolewa kwa njia mwanana ya kuvutia nay a hamasa. Hapakuwa na haja ya kuumwa vichwa ili kuweka vifungu hivyo akilini wala kuhifadhi maji pande ya maneno ambayo yalikusudiwa kubeba uzito Fulani uliolingana na kosa lake. Uhifadhi wake ultumia taswira mbali bali za wadudu, wanyama, ndege, mazimwi, au madude mengine, ambayo waliyapa uhuishi na kuchukua tabia za binadamu.

Ingawa sheia katika jamii za jadi zilitolewa kwa njia mwanana, isije ikaeleweka kuwa watu walikuwa huru kufanya atakalo. La hasha. Kulikuwako na chombo mwafaka cha kuwaadhibu wakosefu. Baraza la wazee kilikuwa chombo mahsusini cha kulinda jamii hizo. Hata hivyo, kiongozi anayehusika hakulazimika kukesha akikariri misahafu ya sheria. Hakuhitaji kewnda na vidokezo vyovoyote kwa madhumuni ya kuvirejelea kila inapobidi.

Kwa upande wa mshtakiwa, moyo wake haukupata kwa ajili ya kiwewe cha yale yatakayofuata. Baada ya kuvutana, alihitajika kuwaomba radhi wazee kwa dhati na kutoa ahadi kutrudia kosa hilo, hivyo kuwaacha wazee kwa dhati na kutoa ahadi kutorudia kosa hilo, hivyo kuwaacha wazee na rajua njema

Ingawaje mashauri yalikuwa yanafanyika kwa njia isiyodhuru, hapakuwa na lelemama yoyote. Mambo hayakuchukuliwa kijuujuu. Ilibidi kutunza wakati barabara. Uropokaji haukuruhusiwa asilani. Mkosaji wa aina hiyo alilipuliwa kwa adhabu. Mara nyingi alitozwa faini ya mifugo, nafaka na hata kufanya kazi maalumu kama vile kurekebisha boma la mikutano, kusafisha josho na mengine.

Mahakama ya kijadi yalifikria uwezo wa mtu binafsi. Aidha, adhabu iliyotolewa kulingana na uzito wa kosa lenyewe. Kwa kuwa ilibidi nidhamu itunzwe wakati mwingine, wazee wa baraza waliweza kubadilisha wale waliokusaidiwa kubarizi. Kwa mfano, katika mashauri yaliyohusu ugomvi-mtu na mkewe hawawi kuwekwa pamija katika baraza moja isipokuwa kwa nadra sana baada ya kila kukosekana.

Katika kuendesha mashtaka, tanzu za fasihi simulizi kama metahli, zilitumika ili kumwangazia mhusika aelee ubaya wa kosa lake, ili afikie majuto ya dhati na ajifunze kuwa raia mwema kama wengine.

Sheria hizo ziliweza kubadilishwa au kufanyiwa mabadiliko ya aina Fulani pindi inapobidi. Kwa mfano, mgeni anapojiunga na jamii, ilibidi baraza la wazee kumjulisha desturi, mila na sheria zote za jamii ile.

Maswali

(a) Je, mwandishi ameonyesha tofauti zozote kati ya mahakama ya kisasa nay a jadi? Fafanua (al.4)

.....
.....
.....
.....
.....

(b) Fasihi simulizi na sheria za jamii za jadi zimeonyeshwa vipi? (al.2)

.....
.....

(c) Unafikiri kulikuwa na upinzani au utetezi katika uendeshaji wa mashataka ya kijai? (al.3)

.....
.....
.....

(d) Kwa ufupi eleza vile mkosaji alivyoadhibiwa kulingana na sheria za jadi (al.2)

.....
.....

(e) Eleza maana ya maneno haya kama yalvyotumiwa katika taarifa (al.2)

(i) Misahifu

.....

(ii) Lelemama

2. MUHTASARI

Soma habari ifuatayo kasha ujibu swalı

Ili kupiga vita propaganda za wakoloni mamboleo katika vyuo vikuu vyetu, inafaa kutumia kiswahili kufundishaji masomo yote. Jambo hili ni lazima na linawezekana kabisa, ingawa lina matatizo yake. Jambo linalotakiwa kufanywa nu kuchukuwa wananchi wenyewe elimu ya juu wakatafsiri fikra za wazalenda katika Kiswahili. Kwa njia hiyo, lugha ya wanachuo itakuwa ndio lugha ile ile ua umma

Na jambo la kuepukwa kwa na lugha mbili ambazo zinasaidia kuwatenga wasomi na umma. Wasomi wetu watakuwa wamekaribia umma kwa kutumia lugha iliyozoleka na umma wenyewe. Jambo linalotutinga ni hili: mara nyingi wasomi wengine waliozoea kutakalamu lugha ya kiingereza wanapajaribu kuwaeleza watu wengine jambo la kielimu au kitaalamu, hushundwa kabisa. Wao huchanganya sana maneno ya kiingereza na Kiswahili hata kufikia kiasi ambacho mtu wa kawaida haelewi chochote.

Kwa kuwa wakoloni-maboleo wameelewa kwamba lugha ni kioo cha kuchujia utamaduni, miaka ya hivi karibuni wamejifunza kwa dhati kuliko mwingine kupigania ufundishaji wa lugha zao, hususani, Kifaransa na Kiingereza. Wakati huo huo wao wanatoa porojo kuwa alugha ya Kiswahili haifai na kwamba ni lugha ya watumwa. Kwa mfano, utaona katika maandishi mengi kila wanapooodhesha lugha kuu za dunia. Kiswahili hakionyweshwi katika hizo.

Badala yake wanaiweka kwenye kiwango sawa na kiganda, kikuyu, Kinyamwezi na lugha kadha wa kadha za kikabila. Hiyo ni harakati kubwa ya kudanganya umma na kuvivua Kiswahili hadhi yake ilhali hii inatumwa na zaidi ya watu milioni mia moja wanaosambaa katika sehemu mbalimbali za ulimwengu. Kwa kutmia hila hii, wao wanawazadikisha watu wengine ili wachukulie Kiswahili kama lugha nyingine ya kikabila. Ndiposa hawa wakoloni-mamboleo wanawashiwishi baadhi ya watumiaji wa kiswahil wastawishe lugha za makabila na kuonyesha kwamba umaarufu wa lugha hizo ni sawa na Kiswahili. Hayo bila shaka ni mawazo hatari. Ukweli uliopo nni kwamba kusema hivyo si kudhalilisha umuhimu wa kukuza lugha za kikabila. Tusemacho ni kuwa ukuzaji wa lugha hizo ungekuwa na kusudi mona kuu ambalo ni kustawisha Kiswahili kufikia ngazi za kimataifa

Swali ambalo ni muhimu kujiuliza ni hili: wakoloni-mamboleo wanatuonaje tunapokazania Kiswahili? Je, wanaona ni faida kwao au kwetu? Jambo muhimu zaidi ni kuambua jinsi Kiswahili kinavyotuonyesha kuungana na kuwa kitu kimoja. Ni dhahiri wakoloni-mamboleo huwfurahii wanapoona Kiswahili kikitunganisha. Machni mwao Kiswahili ni ishara mojawapo ya Kiingereza. Kifaranza au kijerumani, la hasha. Tunachosema ni kwamba tutumie Kiswahili ambacho ni kioo cha utamaduni wetu.

Maswali

(a) Eleza pingamizi zilizowkwa na wakoloni –mamboleo ili kudumisha Kiswahili. (maneno 50-60)

Matayarisho

(al.8,1 yautiririko)

(b) Kulinaga na mwandishi ni sababu gani zinazowafanya Wakoloni-mamboleo kupinga maendeleo ya Kiswahili (maneno 25-30) (al.5,1 ya utiririko)

Matayarisho

Jibu

.....
.....
3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)

(a) *Linanisha na utofautishe sauti zifuatazo*

(al.2)

- (i) /th/, /dh/

(b) *Tambua pasili ya maneno yafuatayo*

Kwanifano shukrani-kiarabu

- (i) Roshani

- (ii) Hundi

(c) *Tunga sentensi inayodhahirisha*

(al.4)

- (i) Nomino ya wingi

- (ii) Kitenzi kishirikishi kuipungufu

(d) *Tumia jozi ya maneno yafuatayo kutunga sentenzi moja*

(al.2)

Fumba na vumba

(e) *Tofautisha matumizi ya ngali katika sentenzi zifuatazo;*

(al.2)

- (i) Wanafunzi wangal wanasherehekeea

- (ii) Wanafunzi wetu wangalsoma wangalipita mtihani

(f) *Tumia ‘O’ rejeshi ili kudhahirisha hali ya mazoea* (al.2)

Mgonjwa ambaye anakula lishe bora ndiye ambaye atapona haraka

(g) *Bainisha aina za virai katika sentensi ifuatayo* (al.3)

Walimshangilia mgeni wao kwa shangwe

(h) *Ainsha viambishi katika neon lifuatalo* (al.3)

Tutakayempiga

(i) *Bianisha aina za yambwa katika sentensi ifuatayo* (al.3)

Mkulima aliyekata nyasi kwa mundu amewalisha punda

(k) *Andika katika usemi halisi* (al.2)

Robi alisema kuwa ilikuwa lazima wao waonyeshe heshima kwa watu wote ikiwa walitaka kuendelea vyema maishani

(i) *Sahihisha sentensi zifuatazo* (al.2)

(i) Mbona haujaenda sokoni

(ii) Penye niliandika ni hapo

(m) *Andika katika ukubwa*

(al.2)

Wazee hawa wana wake na watoto wengi

(n) *Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya visanduku*

(al.3)

Motto aliyekamatwa jana ni mwizi

(o) *Unda nomino mbili kutokana na kitenzi ‘chuma’*

(al.2)

(p) *Andika kinyume cha:*

Furaha anajenga nyumba mjini

(al.2)

(q) *Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli ya kutendeshea na kutendeshwa*

(al.2)

(i) Fa

(ii) Nywa

(r) *Kanusha sentensi ifuatayo*

(al.1)

Ningelikuwa na pesa ningelinunua kitanu kile

4. ISIMU JAMII (Alama 10)

Eleza kwa kutolea mifano dhana zofuatazo

(a) Sajili

(b) Lafudhi

(c) Lahaja

(d) Lingua franca

(e) Krioli